

**MAKAO MAKUU**

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole

S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

## TANGAZO KWA UMMA

**MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA GEITA (GEITA WSSA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21**

**Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-002-2018/2019**

Mnamo tarehe 19 Septemba 2018 Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Geita (Geita WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Majedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

**Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)**

Kundi la Wateja	Bei za Sasa		Bei zinazopendekezwa				
	2017/18	Mabadi liko (%)	2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadi liko (%)	2020/21
Majumbani	390	131%	900	20%	1,080	20%	1,296
Taasisi	430	182%	1,211	30%	1,574	30%	2,047
Biashara	510	216%	1,610	30%	2,093	30%	2,721
Viwanda	-	74%	1,500	30%	1950	30%	2,535
Magati	TZS 50/20ltrs	0%	TZS 50/20ltrs	0%	TZS 50/20ltrs	0%	TZS 50/20ltrs

**Jedwali Na.2: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Mwezi)**

Kundi la Wateja	Tozo za Sasa		Tozo zinazopendekezwa				
	2017/18	Mabadi liko (%)	2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadi liko (%)	2020/21
Majumbani	-	NA	2,000	0%	2,000	0%	2,000
Taasisi	-	NA	2,000	0%	2,000	0%	2,000
Biashara	-	NA	2,000	0%	2,000	0%	2,000
Viwanda	-	NA	2,000	0%	2,000	0%	2,000
Magati	-	NA	2,000	0%	2,000	0%	2,000

**Jedwali Na.3: Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho)**

Kundi la Wateja	Ada za Sasa		Ada zinazopendekezwa				
	2017/18	Mabadi liko (%)	2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadi liko (%)	2020/21
Majumbani	120,000	(58%)	50,000	0%	50,000	0%	50,000
Taasisi	120,000	(58%)	50,000	0%	50,000	0%	50,000
Biashara	120,000	(58%)	50,000	0%	50,000	0%	50,000
Viwanda	120,000	(58%)	50,000	0%	50,000	0%	50,000
Magati	120,000	(58%)	50,000	0%	50,000	0%	50,000

**Jedwali Na.4: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa huduma)**

Kundi la Wateja	Ada za Sasa		Ada zinazopendekezwa				
	2017/18	Mabadi liko (%)	2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadi liko (%)	2020/21
Majumbani	10,000	0%	10,000	20%	12,000	20%	14,400
Taasisi	10,000	0%	10,000	20%	12,000	20%	14,400
Biashara	10,000	0%	10,000	20%	12,000	20%	14,400
Viwanda	10,000	0%	10,000	20%	12,000	20%	14,400
Magati	10,000	0%	10,000	20%	12,000	20%	14,400

**Jedwali Na. 5: Tozo ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuondoa Majitaka kwa Wateja (Shilingi)**

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa		Tozo inayopendekezwa				
	2017/18	Mabadi liko (%)	2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadi liko (%)	2020/21
Majumbani	70,000	0%	70,000	0%	70,000	0%	70,000
Taasisi	70,000	14%	80,000	0%	80,000	0%	80,000
Biashara	70,000	14%	80,000	0%	80,000	0%	80,000
Viwanda	70,000	43%	100,000	0%	100,000	0%	100,000

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Geita imeeleza kuwa bei na tozo zinazopendekezwa zitaiwezesha mamlaka kulipa gharama za uendeshaji na matengenezo, gharama za ukarabati na ununuzi wa vifaa na tozo zilizopo kisheria.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 15 Novemba 2018 katika Ukumbi wa Mikutano wa GEDECO** uliopo Geita Mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Geita na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani

iliyooneshwa hapo juu **ifikapo tarehe 23 Novemba 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA ZIWA, GHOROFA YA NNE, JENGO LA PPF; BARABARA YA KENYATTA, MWANZA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA GEITA**

**Imetolewa na:**  
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**  
**(EWURA)**

**2 Novemba 2018**